

MFUMO WETU WA USAWA WA KIJAMII UNAOLINGANA NA HALI



Mfumo wa Usawa wa Kijamii Unaolingana na Hali ni kanuni za kawaida za kutusaidia kuhakikisha kuwa kila mtu katika jamii yetu ana usaidizi anaohitaji ili kuwa na maisha yenye afya, kujumuishwa na kushiriki kikamilifu.

Mfumo huu utaongoza jinsi tunavyoshirikiana na jamii ili:

- kuboresha usawa kulingana na hali katika jinsi watu wanavyopata huduma na maeneo
- kuboresha afya na ustawi na
- kuleta mabadiliko ya kudumu.

Mfumo huu unaangazia jukumu la haki ya kijamii, usawa unaolingana na hali, utofauti, ujumuishaji na haki za binadamu katika kila huduma na mpango, na kila nafasi na mahali tunaposimamia.

Picha ya 1: Uwakilishi wa picha wa Usawa, Usawa Unaolingana na Hali, Haki

USAWA



USAWA UNAOLINGANA NA HALI



HAKI



Mfumo huu unazingatia maono mahiri na bunifu ya jamii ya miaka 30 na Mpango wetu wa Jamii wa miaka ya 2021–25. Utatusaidia kujenga jamii yenye haki kwa kupunguza vikwazo na kugawana rasilimali kwa haki.

USAWA UNAOLINGANA NA HALI NI NINI?

Usawa unaolingana na hali unahusu kufanya mabadiliko yanayohitajika ili kila mtu aweze: kufikia mipango na huduma; kushiriki katika kazi, elimu, na shughuli zingine; kushiriki maoni yake; na kufurahia kuishi katika jamii hii nzuri.

Tunapofikiria kuhusu usawa unaolingana na hali, tunaweza kuona kwamba watu wana mahitaji, uzoefu wa maisha, viwango vya mamlaka, na athari tofauti kwa maamuzi. Tunahitaji kuzingatia mambo haya na kutafuta njia za kuifanya jamii yetu kuwa ya haki.

Watu wanaweza kukumbana na vikwazo vinavyohusiana na lugha, umri, historia, jinsia au uwezo. Hapo chini kunani baadhi ya maelezo kuhusu watu katika jamii yetu wanaoweza kukumbana na vikwazo.

MAELEZO MUHIMU MAHUASUSI



2,402 (1%) YA WATU WANAJITAMBULISHA KUWA WENYEJI WA ASILI (ABORIGINAL) AU WENYEJI WA VISIWA VYA TORRES STRAIT



6.3% YA WANAWAKE NA **5.7%** YA WANAUME WANAHITAJI MSAADA KUTOKANA NA ULEMAVU MKUBWA AU SUGU.



26.7% YA WATU WAZIMA WANAZUNGUMZA LUGHA NYINGINE ISIPOKUWA KIINGEREZA NYUMBANI



2,026 YA WATU NI WATEJA WAKIMBIZI WA DIVERSITAT



122 KWA KILA WANAWAKE 10,000 NI WAATHIRIWA WA MATUKIO YA UNYANYASAJI WA KIFAMILIA



5% YA WATU WAZIMA WANAJITAMBULISHA KUWA LGBTQI+




13.3% YA IDADI YA WATU INAUNDWA NA VIJANA (UMRI WA MIAKA 15–24)



30% YA IDADI YA WATU INAJUMUISHA WATU WAZEE (UMRI WA MIAKA 55 NA ZAIDI+)

Picha hii inaonyesha jinsi watu wanaweza kuathiriwa na vikwazo katika zaidi ya eneo moja:



JE, MFUMO HUO UTATUSAIDIA VIPI KULETA USAWA UNAOLINGANA NA HALI?

Mfumo huo unazingatia nyanja sita muhimu ambazo zinaunga mkono usawa unaolingana na hali. Hivi ni Viwezeshaji vya Usawa wa Kijamii Unaolingana na Hali vya Jiji.



HAKI

Kusambaza rasilimali na kuwezesha michakato na matokeo ya haki kwa kila mtu.



UFIKIAJI

Kupunguza vikwazo vya kimwili na kijamii kutoka kwa maeneo, nafasi, rasilimali na fursa kwa kila mtu.



MAONI

Kuunda nafasi salama kwa kila mtu kuzungumza na kusikiliza kwa kina mahitaji yao binafsi na ya pamoja.



USHIRIKI

Kumsaidia kila mtu kuhusika katika fursa za kijamii, jamii na kiuchumi.



UJUMUISHAJI

Kuunda fursa ambapo kila mtu anahisi salama, kuungwa mkono na anahisi kuhusishwa, bila kujali utambulisho wa kijamii, sifa au hali zake.



UWEZESHAJI

Kumsaidia kila mtu kufanya maamuzi muhimu na kuchangia katika maamuzi yanayomhusu.

Kwa kuchukua hatua katika kila mojawapo ya nyanja hizi, na kushirikiana na kamati zetu za ushauri na wanajamii, tutaboresha usawa kulingana na hali katika kila kitu tunachoendesha na kusimamia, na kusaidia kuunda jamii yenye haki.

JE, TUTAFANYA HILI VIPI?

KURIPOTI

Tutahakikisha kwamba usawa wa kijamii unaolingana na hali unaboreka kwa kutumia data tunayokusanya ili kuripoti kuhusu Mpango Wetu wa Jamii wa miaka ya 2021–25 na uendeleu.

USHIRIKIANO

Tutashirikiana na kamati za ushauri, vikundi vya jamii na washirika wetu. Pia tutashirikiana na washirika wapya wakati hii itasaidia kufikia malengo yetu.

MATOKEO

Usawa wa kijamii unaolingana na hali utafanya mambo kuwa bora zaidi katika nyanja nyingi za jamii yetu, kama vile kutokuwa na uwezo, afya na ustawi.

UONGOZI

Madiwani na viongozi wetu watahakikisha kwamba usawa wa kijamii unaolingana na hali ni sehemu ya maamuzi yote kuhusu huduma, mahali, matumizi na upangaji.



Picha iliyo hapo juu: Vijana wakisoma pamoja kwenye maktaba

KITUO CHA HUDUMA KWA WATEJA

100 Brougham Street,
Geelong VIC 3220
8:00asubuhi – 5:00jioni

© City of Greater Geelong 2022

CITY OF GREATER GEELONG

WADAWURRUNG COUNTRY
SANDUKU LA POSTA 104, Geelong VIC 3220
Simu: 03 5272 5272

Barua pepe: contactus@geelongcity.vic.gov.au

HABARI ZA HIVI PUNDE:

[f CityofGreaterGeelong](https://www.facebook.com/CityofGreaterGeelong) [@CityofGreaterGeelong](https://www.instagram.com/CityofGreaterGeelong)
[t @GreaterGeelong](https://www.twitter.com/GreaterGeelong) [in CityofGreaterGeelong](https://www.linkedin.com/company/CityofGreaterGeelong)

www.geelongaustralia.com.au